

Mhe. Ramadhani Shaabani Abdallah – Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Katiba na Utawala Bora, alianza kwa kuelezea furaha yake kuona mkusanyiko huu unahusisha Tanzania nzima. Ni furaha inayoonyesha Watanzania wanashirikiana pamoja na mafanikio yanapatikana. Fanyeni kazi pamoja na Muungano utadumu. Nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wa Bodi kwa mwaliko huu adhimu wa kufungua Tamasha la AZAKi, 2009. Ni heshima kwangu na pia kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwani huu ni mwaliko wa kwanza kabisa wa Waziri kutoka SMZ.

Tamasha hili lina malengo makuu matatu ambayo ni:

- AZAKi kutafakari mafanikio na changamoto za MKUKUTA/MKUZA
- Kutambua AZAKi zinazofanya vyema shughuli zake
- Kukuza Taswira njema ya AZAKi – kwa kuzijengea uwezo

Ni furaha kubwa kwangu kuona Tamasha linawaleta pamoja wasomi, Serikali, Taasisi, Sekta Binafsi na ninyi AZAKi na kufanya tafakari ya jinsi AZAKi zinavyokua na kusonga mbele zaidi katika mchango wake wa kuondoa umasikini. Kauli Mbiu ya mwaka huu ni *“Tathmini ya Ushiriki wa Wananchi katika Utekelezaji wa MKUKUTA/MKUZA”* Hili ni jambo linalosaidia Serikali zote mbili, SMZ na Serikali ya Muungano ambazo zinathamini mchango wa AZAKi katika kuondoa umasikini. Wananchi wakishirikiana na AZAKi na vikundi vingine vya kijamii, wamekuwa wakishiriki katika michakato mbalimbali ya maendeleo yao. Serikali zote zinatambua nafasi ya AZAKi katika kupunguza umasikini, na huu ni muda muafaka wa kufanya tafakuri ya changamoto na mafanikio yaliyopatikana katika MKUKUTA/MKUZA. Tathmini za utekelezaji zinazofanywa na tafiti nyingine zitasaidia serikali zetu ziandae mipango bora zaidi ya programu hizi. AZAKi zinao mchango mkubwa katika utawala shirikishi; mijadala ya utawala bora, haki za jamii zitajenga hamasa kwenu kuendelea kuwatetea wananchi.

Changamoto yangu kwenu, mjiulize maswali yafuatayo:

- Je, ni kwa kiasi gani AZAKi zimesaidia kukuza haki za binadamu na utawala bora?
- Je, ni kwa kiasi gani AZAKi zimesaidia mchakato na Serikali za Mitaa na kushawishi mabadiliko ya sera?
- Je, ni kwa kiwango gani AZAKi zimesaidia uwajibikaji na uwazi katika Serikali?

Nikiwa Waziri mwenye dhamana ya Utawala Bora, ninaelewa kwa kina kazi za AZAKi hasa haki kwa makundi maalumu. AZAKi zielekeze nguvu kwa wale wenye mahitaji

maalumu, kwani hii ndiyo shabaha ya kuanzisha AZAKi. Uhusiano wa AZAKi na Serikali zote mbili zimezisaidia Serikali zetu kujiangalia na kujikosoa. Sekta ya Asasi za Kiraia inapaswa kuwa mfano wa utawala bora. Je, ni kwa kiwango gani AZAKi zimewajibika kwa jamii, wanachama, Serikali na Wafadhili? Je, miundo yetu inaruhusu uwazi? Ni matumaini yangu kwamba jitihada za kuzijengea uwezo AZAKi zitaendelea, kwani hii ndio chachu, bila kuzijengea uwezo asasi hizi kazi ya kuondoa umasikini itakuwa ngumu. Naipongeza The Foundation kwa juhudi zake za kujenga uwezo wa AZAKi. "Nawashukuru tena kwa kunikaribisha katika sherehe hizi. Baada ya hayo, natamka kwamba Tamasha la Saba la Asasi za Kiraia limefunguliwa rasmi. Ahsante sana!"